

Epuka desturi za biashara zisizo za haki

Karatasi ya ukweli kuhusu haki zako za ununuzi chini ya Sheria ya Watumiaji ya Australia

Kama mtumiaji, umelindwa dhidi ya desturi za biashara zisizo za haki.

Tabia ya kupotosha au ya ulaghai

Tabia ya kupotosha au ya ulaghai ihusisha na matangazo, ukuzaji, nukuu, taarifa na uwakilishi ambao unaunda wazo la kupotosha kati ya watumiaji wengi kuhusu bei, thamani au ubora wa bidhaa au huduma za watumiaji.

Kimya

Biashara inaweza kuvunja sheria kama haitashiriki maelezo muhimu kuhusu bidhaa au huduma.

Biashara inaweza kuvunja sheria kama haitashiriki maelezo muhimu kuhusu bidhaa au huduma.

Ubashiri/maoni

Ahadi, maoni na ubashiri unaweza kuwa wa kupotosha au wa ulaghai kama mtu anayetoa taarifa hiyo alijua kwamba sio ya kweli, hakujali kama ilikuwa ya kweli au la, na/au hakuna na misingi yoyote inayoeleweka ya kuitoa taarifa hiyo.

Kanusho na chapa ndogo

Biashara haiwezi kutegemea chapa ndogo kama fursa ya kukupotosha au kukudanganya. Kweli zozote muhimu kuhusu bidhaa au huduma zinapaswa kuonyeshwa wazi wazi na vizuri.

Uwakilishi wa uongo au wa kupotosha

Biashara haiwezi kufanya uwakilishi wa uongo au wa kupotosha kuhusu bidhaa au huduma kuhusiana na:

- bei au thamani, kipimo, umri, mahali asilia, ubora au kiwango
- mtindo wa vijenzi, mfano au historia ya bidhaa
- shuhuda kutoka kwa watu wanaozinunua au kuzitumia
- upatikanaji wa suhula za kurekebishia au vipuri
- ufadhili, uidhinishaji, hali ya utendajikazi, vifaa vya ziada au faida za matumizi
- hitaji la mnunuzi la bidhaa hizo
- dhamana lolote, hati ya kutengeneza au kubadilisha bidhaa yoyote au sharti ya bidhaa hizo.

Ni kinyume cha sheria pia kwa biashara kutoa fidia, zawadi au tuzo bila kukusudia kuzitoa, au kutokuzitoa kama ilivyosemekana.

Tangazo la chambo

Kwa mfano, muuzaji wa elektroni anaendesha kampeni kuu ya utangazaji ya runinga za inchi 42 kwa bei iliyopunguzwa, kwa mauzo ya wiki moja.

Muuzaji huyo kwa kawaida huuza karibu runinga 20 za aina hii kwa wiki, hata kwa bei kamili. Hata hivyo, kwa wiki hiyo ya kampeni, muuzaji ana runinga mbili tu dukani na anakataa kuagiza na kumuuzia mtumiaji runinga kwa bei hiyo iliyopunguzwa.

Hii itazingatiwa kuwa tangazo la chambo kwa sababu muuzaji huyo aliendesha tangazo ambalo liliwahimiza watumiaji kuja dukani, lakini hakuwa na runinga za kutosha ili kufikia hitaji lililotarajiwa.

Kukubali malipo kwa njia isiyofaa

Biashara haiwezi kukubali malipo kwa bidhaa au huduma kama haikusudii kuziwasilisha, au kama haiwezi kuziwasilisha kwa muda unaofaa.

Kwa mfano, msanifu wa mandhari anakubali kuweka mawe ya manjano ya kutengeneza njia na anapokea malipo, akijua kwamba mawe ya kijivu tu ndiyo yanayopatikana.

Nchi asilia ya bidhaa

Biashara haiwezi kunena kwa dhati ya uongo au ya kupotosha kuhusu kama bidhaa zilitengenezwa, kuzalishwa au kukuzwa katika nchi fulani.

Hii inajumuisha:

- 'imetengenezwa katika' au 'imeundwa katika' nchi fulani
- 'zao la', 'bidhaa ya ' au 'imezalishwa katika' nchi fulani
- utumizi wa nembo, kwa mfano, nembo ya 'Imetengenezwa nchini Australia'
- madai kwamba bidhaa, au viambatanisho au vijenzi, 'vilikuzwa katika' nchi fulani.

Kwa mfano, kama furushi la bidhaa linadai kwamba ni 'Zao la Australia' inamaanisha kwamba viambatanisho vyote muhimu vya bidhaa hiyo, na uzalishaji au utengenezaji wa bidhaa, lazima uwe umefanywa nchini Australia.

Karatasi ya kweli

Bei Mbalimbali

Bei mbalimbali ni wakati biashara inaonyesha bidhaa ikiwa na zaidi ya bei moja. Kwa mfano, bei kwenye rafu huenda ikawa tofauti na ile iliyotangazwa kwenye katalogi. Hii ikifanyika, biashara hiyo lazima iuze bidhaa kwa bei ya chini zaidi au iache kuuza bidhaa hadi kosa la bei litatuliwe.

Bei Moja

Biashara hairuhusiwi kutangaza au kusema bei ambayo ni sehemu tu ya gharama, isipokuwa iwe inatangaza pia kidhahiri bei yote kwa jumla.

Kwa mfano, tangazo la katalogi la seti ya viti vya kupumzikia linasema bei kuwa "malipo 6 rahisi ya \$300". Bei ya jumla ya \$1800 imeonyeshwa, lakini iko katika chapa ndogo chini ya tangazo na imefichwa na picha ya viti hivyo. Bei moja ya \$1800 haionekani vizuri kama \$300 na kwa hivyo kuna uwezekano kwamba ni kinyume cha sheria.

Je, tabia isiyofahamika ni gani?

Tabia isiyofahamika ni taarifa au tendo ambalo halifahamiki kabisa, linakiuka ufahamu mwema.

Mifano ya tabia isiyofahamika inajumuisha biashara:

- kutofafanua mkataba vizuri kwa mtumiaji ambaye wanajua hazungumzi Kiingereza
- kumlazimisha mtu kutia saini mkataba ulio wazi au usiomfaa kabisa
- kutumia fursa ya hali hiyo ya mtumiaji, kama vile mahali pa mbali,
- kutumia mbinu za kushinikiza sana kama vile kukataa hapana kama jibu.

0285FT 2012

Kwa maelezo zaidi, wasiliana na wakala wa eneo lako wa kulinda watumiaji. Kwa usaidizi wa lugha piga simu kwa 13 14 50 (uliza mkalimani katika lugha yako).

Australian Capital Territory

Office of Regulatory Services T. (02) 6207 0400

New South Wales

NSW Fair Trading T. 13 32 20

Northern Territory

Consumer Affairs T. 1800 019 319

Queensland

Office of Fair Trading T. 13 QGOV (13 74 68)

South Australia

Consumer & Business Services T. 13 18 82

Tasmania

Office of Consumer Affairs & Fair Trading T. 1300 654 499

Victoria

Consumer Affairs Victoria T. 1300 55 81 81

Western Australia

Department of Commerce T. 1300 30 40 54

Tume ya Australia ya Mashindano na Watumiaji ina jukumu la kitaifa kwa ushindani, biashara ya haki na ulinzi wa watumiaji na unaweza kuwasiliana nao kwa 1300 302 502.